# MUNGU YUKO NYUMA YA KILA JAMBO

***Warumi 8:28-30" Nasi twajua ya kuwa katika mambo yote Mungu hufanya kazi pamoja na wale wampendao katika kuwapatia mema, yaani wale walioitwa kwa kusudi lake.Maana wale aliowajua tangu asili, aliwachagua tangu asili, wafananishwe na mfano wa mwana wake,ili Yeye awe mzaliwa wa kwanza miongoni mwa ndugu mwa ndugu wengi. Na wale aliowachagua tangu asili, hao akawaita na wale aliowaita,hao akawahesabia haki, na hao aliowahesabia haki, hao akawatukuza*.**

Sikiliza kile Nabii wa Mungu alichosema kuhusu hilo: Mungu ana wakati na sababu kwa huo wakati kutimiza haki zake zote. Mungu anajua hasa kile anachoenda kukifanya.Sisi hatukijui. Inabidi tuyapokee kwa kadiri Anavyotupa sisi. Lakini yeye anajua, na hakuna kitakachofanyika kimakosa kwa yale aliyoyapanga kuyafanya.lazima yote yaende hivyo.lazima kuwe na saa ngumu wakati mwingine. Na mambo magumu ili tuu hasa kuonyesha asili halisi ya kile kitu
***(2 Kor.5:7-15).***

unajua mvua inazaliwa katika msukosuko,mgumu wa umeme wa radi,ngurumo angani.Na hatungekuwa na mvua, hatungeweza kuishi.Lakini unaona kile kinachohitajika ili kuleta mvua?Ngurumo,umeme, kumulika kwa hasira, na kutokana na hayo inakuja mvua.
Mbegu inabidi ife, ioze, iharibike, inuke na iende tena katika mavumbi ya dunia ili kuweza kuleta maisha mapya.

Inahitajika kupigwapigwa kwa dhahabu, igeuzwe na kugeuzwa mbele na nyuma na kupigwa mpaka ule uchafu wote utoke.Siyo kwa sababu ina ng'ara kwa sababu madini yaliyochanganyika na chuma ambayo huitwa dhahabu ya mpumbavu hung'ara zaidi kama dhahabu halisi, lakini ulivichanganya hivyo viwili pamoja………..ukiviweka pembeni ni vigumu sana kuvitenganisha lakini ukiviweka pamoja, unaweza kuvitofautisha. Na yule anayeipiga dhahabu hupiga mpaka aione sura yake ikiahisiwa katika ile dhahabu (***1Petro1;6 -7***)
Na Mungu anaweka muda na ana kusudi kwa kila kitu anachokifanya. Hakuna chochote kinachotokea kwa bahati mbaya kwa wale wampendao Bwana nao wameitwa sawa na mwito wake. Unaona tumechaguliwa mbele ***(Waefeso1;3-6)*** na kila kitu hutendwa sawa na hivyo, kila kitu kina wakati wake, kina msimu wake na kina msimu wake na kina njia yake, na Mungu yuko nyuma ya kila litendekalo ***(Zaburi35:6)*** na wakati mwingine unafikiri kila kitu kinaenda vibaya. Hilo ni kwetu sisi, hayo mambo yanawekwa kwa ajili yetu,Majaribu na mambo ya kutuchanganya ni majaribio tu. Ni kwa namna gani tutatatenda kwa yale yaliotokea /hutendeka ***(1Petro4:12-16)*** [1]
Hili Kanisa limeweka hapa kusudi. Iko Roho nyuma yake. Hili kanisa.Roho nyuma ya nyumba yako nyuma ya hili jengo. Nyuma ya kila kitu kuna Roho, kusudi na lengo, hili Kanisa linakuja hapa kwa ukuu wa kumuinua mtu flani au utaratibu flani au kitu flani. Hapo sasa kusudi lake sio sahihi lakini kama limewekwa hapa kujaribu kutimiza kusudi flani kwa ajili ya ufalme flani kwa ajili ya ufalme wa Mungu,hapo sasa kusudi na lengo,vyote ni sahihi.limechunguzwa namna hiyo kuna sehemu ya neno ilioyowekwa kwa kila wakati.na kuna upako flani unaonyesha chini ,ambao unadhihirisha au kulitambulisha ile sehemu ya ile neno ilio weka kwa huo wakati, sasa

unaona pale tulipo leo Sasa tuone hili tunacho paswa kukifanya,hapo sasa ndio utajua tukio umbali gani.Ninaona tu kitu kimoja kilichobaki, na kule kuja kwa Bwana Yesu, wakati wowote,kule kunyakuliwa kwa kanisa, na tunaenda kumulilia yeye Mawinguni.sasa haya mambo inabidi yatimie katika siku hii ya leo,kama tu yeye alivyo ahidi hilo.Atalifanya hilo. [3]

Uzoefu wa Mkristo msingi wake hauko hasa kwa ujumla wake ni katika kutulia (**4:1-3)** "njooni kwangu nyinyi msumbukao na wenye kulemewa na mzigo, Nami nitawapuzisha ***"(Matayo11:25-30)*** tunapelekwa huku na huku na vitu vyovyote mpaka unapokuja kwa Kristo, hapa sasa yote yanakua yameisha. Kupuzika ndani ya Kristo, kikamilifu.Haijalishi kuna kuja nini kunatokea nini,hakuna kiwezacho kutugusa kabla mpaka kwanza kije kwa mchungaji lazima aniruhusu hilo.Biblia ilisema'' katika mambo yote Mungu hutenda kazi huwapatia mema wale wampendao'' lazima lije kwanza kwa mchungaji.Alisema "Mimi ni mlango'' ***(Yohana 10:1-5)*** ''Hakuna mtu awezaye kuja ndani bila mimi kumkubali kwanza ***(Yohana 6:44).*** Ngoja nikwambie hili kuwa Mungu anaporuhusu jambo lolote, linatenda kazi kukupatia mema .Hivyo ndivyo ilivyo hata magonjwa ni hivyo hivyo? Hakika ili Mungu akuponye akupe ushuhuda mkubwa.Akupe kitu Fulani kuendelea mbele nacho''mambo yote hutenda kazi pamoja kukupatia mema''(warumi 8:28-30) [4]
Hakuna kitu chochote kiwezacho kukudhuru wewe, hakuna kiwezacho kukupata ila kile ambacho Mungu amekiruhusu hicho. [5]

Mungu anapokuja ndani ya mtu,au kwa watu,katika kusanyiko,katika mwanaume au mwanamke,Anathibitisha uwepo wake.Mungu anathibitisha kuwa yuko pale.kwanini, mungu anapokuja,ishara za kimbinguni huanza kutokea.Huyu mtu anakuwa mtu aliye badilika.Hawako tena vile walivyozoea kuwa.Dhambi imepotea au imehama katika maisha yao. Woga na shaka havipo tena,kuchanganyikiwa.Wao wako imara,waliosimama wakiwa hai au maiti ni kristo ***(Warumi14:8).***Hawajali kunakuja nini au kunaendelea nini, hakuna cha kuwatetemesha wao. Wanasonga mbele. [6]

Ni saa hizi za muhimu zinazotusukuma kwenda katika michanga ile mitakatifu. Ilikuwa katika Biblia. Nakumbuka,haijalishi misukosuko ni mikuu kiasi gani, shetani hawezi kuchukua uhai wako mpakaa Mungu amemaliza na wewe ila kile ambacho Mungu amekiruhusu na ni kwa kukupatia mema. Hebu tufikiri pale gharika ilipokuja kuharibu ulimwengu haingeweza kumwangamiza nuhu.Nuhu asingeweza kuangamizwa, kwa sababu Mungu alikuwa na kazi ya kufanya Nuhu. [7]

Sasa,huyu mtu kipofu alikuwa ameketi pale, na Yesu na wanafunzi wake wakaja pale, na nafikiri Yesu aliwapa funzo dogo pale.Walipomuona maskini mtu huyu kipofu waliwaza''vema, sasa hakika kuna dhambi pale mahali Fulani ''Tunapoona kitu Fulani kikitokea kwa Mtu mara nyingi tunasema vema''ametenda dhambi, aliondoka katika mapenzi ya Mungu mahali fulani'' Ndugu krase alipogonga nguzo,alikuwa nje ya mapenzi ya Mungu mahali Fulani hayo ni mawazo ya mtu fulani.Wakati bunduki iliponilipukia mimi,''vema, alikuwa nje ya mapenzi ya Mungu'' Ndugu Neville alipogonga gari'' alikuwa nje ya mapenzi ya Mungu''.Hiyo sio hasa hilivyo, hapana bwana siyo hivyo Mungu huruhusu mambo haya ***(Mithali 16:4)*** [8]

Lakini wakati mwingine Mungu huweka magonjwa juu yetu kutufanya tujue kuwa yeye bado ni mtawala wa maisha yetu.Na tuko hapa kwasababu tuu ameruhusu sisi kuwa hapa, na ni neema yake kwamba tuko hapa na tunalazimika kumtumikia yeye (***Joshua 24:15)*** [9]

Kwa utaratibu wa mashariki wa zamani, jinsi walivyowaangalia kondoo wao, Yule mchungaji anawaingiza ndani usiku, na anawahesabu mmoja kuhakikisha kila moja yupo, kama kuna

anayekosekana, hatalala mpaka iende huku jangwani na porini au popote pale alipochungia siku nzima, naye atampa Yule kondo na kumuweka juu mabegani mwake, na kumleta ndani. Wote wanapokuwa zizini hapo sasa mchungaji anajilaza mwenyewe pale mlangoni. Yeye ni mlango wa kuingilia kwenye zizi. ***(Yohana 10:1-10)*** hakukuwa na njia nyingine, kaupenyo ambako juu kana ufuniko. Na hakuna chochote kinachoweza kuwafikia kondoo. Bila kuanza kwa Mchungaji.

Ni faraja ya namna gani, ni ktu kizuri namna gani, kujua kuwa tunapoingizwa katika hifadhi yake iliyobarikiwa. Na Yeye anakuwa mlango, na hakuna chochote kinachoweza kukupata wote, haijalishi ni nini, vyote lazima vipitie kwa mchungaji, kama ni ugonjwa, ni kwa ajili ya kukusahihisha, inaweza ikawa ni ushuhuda kwa ajili ya kwenda kinyume na adui. Inaweza ikawa ni kusudi la kulinua jina la Kristo, lakini hakuna kiwezacho kuja kwako mpaka yeye amekiruhusu kije. yeye ni mlango wa kondoo.

Vyote vinavyokuja kwa yeye ili vije kwako, kujaribu kukuondoa katika zizi lake ni (wezi na) wanyang'anyi, wake waovu … lakini hawawezi kukupata wewe. Hakuna kinachoweza kukupata wewe, hakuna kinachoweza kukusumbua wewe kama uko katika zizi la Mungu kwa sababu yeye mwenyewe ni mlango, na hakuna njia nyingine, kila kitu ni lazima kiruhusiwe na yeye
***(2 Kor 4:15).*** [10]

Hakuna kitakachowasumbua hawa wadogo, Yeye ataenda kulishughulikia hilo, hakuna kitakachoenda kukusumbua wewe, usiwe mwoga kumchukua Mungu katika Neno Lake. Wewe tulia tu na uwe na imani na uamini kuwa yeye anakuangalia wewe, ataenda kukiangamiza kukitowesha chochote ambacho kinakusumbua wewe. Ooh! Ambacho kinawea kukushambulia wewe. Lakini hakiwezi kukuumiza wewe.

Kwa maana mambo yote, anayaruhusu Yeye, haiwezi kuwa vinginevyo, kwa maana inatenda kazi pamoja na wale wampendao bwana katika kuwapatia mema. Na hakuna chochote cha kukuumiza kitakachokufikilia wewe [11]

Mungu analeta mivutano ndani ya kanisa, kwa maana kila mwana amjuaye Mungu ni lazima ajaribiwe kuthibitishwa, na hupewa mtihani ***(Waebrania 12:4-11)*** anaruhusu maumivu yakupate wewe. Anaruhusu magonjwa yakujie wewe kukupima na kukuthibishia wewe. Kuonyesha dunia kuwa wewe ni mzawa wa Ibrahimu. Anayeruhusu hayo kwa mapenzi yake mwenyewe anaruhusu magonjwa, anaruhusu marafuki kinyume na wewe. Anaruhusu mambo hayo tena anamfungulia shetani akujaribu wewe, na atakufanyia yote ila tu asichukue uhai wako. Anaweza kukupata kwenye kitanda cha mateso; anaweza kuliachia kanisa liwe kinyume na wewe, anaweza kufanya karibu kila kitu na ni mapenzi ya Mungu afanye hivyo. Tunamfundisha kuwa , ni ya thamani sana kwenu kuliko dhahabu ***(1 Petro 1:3-9)*** [12]
Wakati mwingine unasema "kwa nini mnakuwa wagonjwa?" inaweza kuwa kwa ajili ya utukufu wake wakati mmoja walipokuwa wanampitia mtu kipofu, wanafunzi walisema, " nani alitenda dhambi, huyu mtu au mzazi wake? ***(Yohana 9:1-4)*** na Yesu alisema " katika hali hii hakuna aliyetenda dhambi, yeye au wazazi wake. Lakini ni ili kazi za Mungu ziweze kudhihirika" [10]

Siyo jambo la ajabu jinsi Mungu anavyowaacha watoto wake waende mbali mpaka hatua ile ya mwisho? Oh wakati mwingine anaruhusu hilo ili kuona mtu utavyofanya. Biblia ilisema"kama hatuwezi kustahimili madai ya Mungu, kwa hiyo tumekuwa wana wa haramu na sio watoto wa Mungu!! Tumezaliwa kwa Roho wa Mungu. Imani yetu kwa Mungu inashikilia neno lake, imewekwa katika neno lake na hapo inashikilia. [13].

Wakati mtu fulani anapoanza kukudhihaki wewe na kusema kwa mtindo wa kale, mwangalie Yeye ni Oh! mliwaambia ninyi amezoea kuwa…………. Oh hivyo ni sawa tuu, hayo ni maumivu ya kukua, hayo ndiyo yale maudhi ambayo ni mazuri kwako. Ni maumivu ya kukua.

Oh!, ndiyo , anaruhusu ukutane na njia zikatizazo jia panda, mara nyingi hufanya hivyo ili atukamilishie sisi kwa huduma. Anaruhusu hayo mambo yatoke. Je huelewi hayo? Anafanya hayo ili akuelimishe kwa wito ule aliokuitia wewe. Hayo ni maumivu yako ya kukua. Aliyemfanyia Daniel hivyo mnajua aliwafanyia wana kiebrania, katika tanuru la moto
(***Daniel 3).*** Lile tanuru la moto lilifanya nini? Tanuru la moto lilifanya vifungo vilivyowafunga, hivyo ndivyo tuu. Tanuru la moto lilivyofanya liliunguza tu vifungo vilivyokuwa vimewafunga [14]
Na wakati mwingine ilichukua majaribio magumu kuvunja vifungo vya dunia vilivyotufunga
(***1 Petro 4:1-2)*** wakati mwingine Mungu anatuachia tupitie majaribu kidogo. ***(1Kor 10:12-13)*** unajua, na kuona tutafanya nini, kukutoa wewe katika ulimwengu, Or kwa maneno mengine, anakuacha wewe upate majaribu kidogo na kukutoa nje ya hilo dhehebu, na hilo wazo la wamethodisti ndio pekee. Walilonalo. Kama huwezi kuliamini hili kama kanisa langu linavyoliamini hilo kwamba huamini kabisa" wakati mwingine anaacha majaribu kidogo yatokee. Pengine una mtoto mgonjwa, pengine jambo fulani linatokea pale katika saa ya kufa. Pengine mtu fulani ameondolewa kutoka kwako, au kitu fulani. Inafanya nini hiyo? Kukuvunjavunja, kukuonyesha wewe kitu fulani, kufungua macho yako. Pengine umekuja kutoa shutuma, wakati mwingine, pengine Mungu anafanya hivyo kuvunja vifungo vya dunia vilivyo kufunga wewe.

Kama mtu anayezama majini/mtoni, inabidi umtoe yule mtu mtoni kabla ya kuutoa huo mto ndani ya huyo mtu. Hiyo ni sawa. Umtoe mtoni kwanza, halafu unatoa mto kutoka ndani yake. Wakati mwingine Mungu humfanya hivyo anaruhusu njia panda, barabara za kupishana na nyingine. Simama katika ahadi zake, lile neno. Kwa maana kamwe halishindwi. Mambo ya mbele, simama katika ahadi zake, lile neno. Kwa maana kamwe halishindwi mambo ya mbele, yako mkononi mwake. Simama kama walivyofanya, usiachilie ***(Ayubu 23:14).*** [15]

Mwangalia Ayubu, mtu mkamilifu, mtu mwenye haki na Mungu alimruhusu mwovu shetani ili amjie yeye, na kumrudi yeye, na kila mkitufanya kwa ajili ya kukamilisha Roho yake Mungu hutumia roho wabaya mara nyingi ili kuweza kutimiza mpango wake wa mapenzi yake.
***(Zaburi 105:17-19; Daniel 1:1-2)*** [16]

Lakini watu kama hawatatembea katika mapenzi yake makamilifu, yeye anayo mapenzi ya kuachilia, atakuachia utembee katika hayo. Lakini ataacha itende kazi kwa ajili ya utukufu wake. Katika mapenzi yake makamilifu.

Kama tu ilivyokuwa pale mwanzo, haikuwa ni mapenzi makamilifu ya Mungu watoto wazaliwe duniani kwa njia yan kujuana kimwili. ***(Mwanzo 1:26-28)*** hapana bwana. Mungu alimuumba mtu kutoka mavumbi ya nchi. Akapulizia pumzi ya uhai ndani yake, naye akawa nafsi iliyo hai. Kutokana na huyu mtu alitoa msaidizi na akamfanya awe mke wake, hiyo ilikuwa ni mapenzi ya kwanza ya Mungu, na dhambi ilipoingia na kufanya mambo aliyofanya, ndipo aliporuhusu mtu aoe mke kihalali na kupata watoto kupitia yeye, "zaeni mkaijaze nchi, kama hiyo ndiyo njia mtapitia kufanya hivyo." Lakini unaona haikuwa kamwe mapenzi yake makamilifu.
Mungu aliwaruhusu Israeli wachukue sheria, katika kutoka sura ya 19. Wakati neema tayari imewapa wao nabii, nguzo ya moto, kondoo wa sadaka, nguvu ya kukomboa lakini walimlilia

wapewe sheria. Haikuwa ni mapenzi ya Mungu lakini illiingizwa kwa sababu watu walihitaji hiyo. Nao wakalaaniwa na sheria ileile walioitaka.

Ni bora/vizuri sana kupata mapenzi ya Mungu. Hivyo ndivyo alivyotufundisha. "Mapenzi yako yafanyike, ufalme wako uje, mapenzi yako yafanyike" ***(Mathayo 6:9-15)*** ni lazima tujisalimishe wenyewe kwenye mapenzi yake. Na Neno Lake. Usilihoji au usiliulize maswali. Liamini hilo,usijaribu kulitafutia njia kulizunguka hilo! Lichukue vile lilivyo, Wengi wanapenda kwenda kinyume hivyo unajiona wewe mwenyewe unaendelea unamuona Mungu anakubariki. Lakini anatenda kazi katika mapenzi ya kuachilia sio katika mapenzi yake makamilifu mapenzi yale kiungu Analiruhusu hilo kama nilivyosema lakini haliachi hilo liwe mapenzi yake makamilifu lakini atalifanya hilo litende kazi kulituliza na kubariki mapenzi yake makamlifu na kuzaa watoto kwa hujuana kimwili ni moja ya mambo hayo. [17]

Kwa hiyo tunamuamini kabisa kuwa Mungu kamwe habadili mawazo yake juu ya kile alichosema .siku zote ni kweli analifanya hivyo. Lakini anayo mapenzi kuachilia. Sasa hapo ndipo tatizo lilipo.Tunajaribu kufanya kazi katika ya kuachilia na Yeye ataniruhusu hilo.Lakin pia kama tulichukua mapenzi yake ya kuachilia ingawaje siyo sahihi Atayafanya mapenzi yake ya kuachilia yatende kazi pamoja hutukuza mapenzi yake makamilifu .

Lakini anaona Mungu yule Roho mkuu yule Baba ***(Yohana4:24).*** Ndani yake mna sifa mambo anayoyaona yalidhihilishwa sasa zile sifa zake. ambazo zinadhihilishwa.Aliishi peke yake yeye alikuwa hata sio Mungu ,Mungu ni kiumbe kinachoabudiwa. Yeye alikuwa mkuu wa milele.na ndani yake kulikuwa na sifa. Kama vile kuwa baba kuwa mwokozi kuwa mponyaji. kwanza kwa imani gani na sasa angeweza..Alipaswa awe baba kwani inathibitisha Yeye alikuwa baba .Lakini yu aishi pale yake.Yeye pekee ndiye asiyepatikana na umauti . na sasa zile sifa zake inabidi zidhihirishwe.

Sasa kuwa mwokozi lazima kikiwepo kitu kilichopotea .na huweza kupoza kwa makusudi halafu akikomboe hicho haitakuwa inafaa kwa utakatifu wake na huo ukuu wake wa maamuzi. Lakini amemuweka mtu katika uhuru wa kuchagua alijua kwamba mwanadamu angeanguka. Na katika hilo sasa alikuwa mtu, yeye mwenyewe kumkomboa mtu aliye anguka. Hiyo ndiyo sababu Yesu amekuwa Emmanueli ***(Mathayo 1:1-23).*** kama Mungu angetuma mtu mwingine mbali ya Yeye mwenyewe na sasa hiyo ingekuwa haki . Mungu ilibidi aje mwenyewe na kuchukwa nafasi . Na Mungu asingekuja katika mwili huku chini na kuchukua nafasi .na nafasi ilibidi ifanyike mwili kati mwili wa mwana wake mwenyewe aliyemuumba ***(ITimetheo 3:16,filip2:5-11)***

Na ameonyesha hapa tangu mwanzo ya kuwa mapenzi lakini aliruhusu kujuana kimwili kuingie. Kamwe yeye lakini hakukusudiwa hilo la watoto kuzaliwa kwa kujuana kimwili lakini aliyaruhusu kuyaachilia ambayo kitambo kidogo tuu yatakayotoweka. [18]

**Nukuu za kiingereza**:

- shutma kwa ajili ya neno(63-1223)aya 11
- ushuhuda (63-1128m)aya 26-29
- uzoefu (52-0726)aya ya 5
- ushirika (56-0212) Aya E 31
- Kutokukosea kwa Mungu neno lililonenwa (56-0404) Aya E35
- Kwa nini unalia nena (59-1004E), Aya E15
- Ninajua (60-0417S) Aya 36
- Kuchukua upande pamoja na Yesu (62-0601) COD uk 775
- Yale maandiko kwenye Ukuta (56-0308) Aya E 32
- Mchungaji mwema wa kondoo (57-0308) Aya E-11-E-12
- Isikie sauti yake (58-1005M), Aya E 79
- Kumiliki malango ya adui (59-1108), Aya 35.
- Kuwa na hakika na Mungu 59-0708 E Aya 28
- Shalom (64-0119), Aya 180-182
- Shalom (64-0112), Aya 227- 228
- Maswali na majibu juu ya Roho mtakatifu (59-1219) COD uk Aya 104-432
- Je Mungu hubadili maneno yake juu ya neno lake 65-04181E Aya 92-98
- Je Mungu hubadili jia yake (65-0427) Aya 45-51

Jiwe la kiroho la kujengea No. 21 mpya 2010) kutoka kwenye neno lililofunuliwa la saa, Imekusanywa na Gerd Rodewald Friedsfr.69,D-75328 Schomberg, Germany
www.biblebelievers, Fax(+49)72353306

---

Anakuja mmoja na ujumbe ambao ni moja kwa moja ni Biblia na kazi ya haraka itazunguka dunia. Na mbegu zitaingia magazetini, vitu vya kusomea, mpaka kila mbegu iliyokusudiwa kimbele imesikia.

(Ndugu Branham katika mwenendo utaratibu na mafundisho uk 724

*Kwa nakala zaidi za kiingereza au kiswahili Andika kwa:*

*Charles E. Y. Kanju,*

*Box 553 Korogwe - Tanga*

*E-mail: Chaelika@livel.com*

*Cellphone: 0784 704299/ 0718230098*